**East African Journal of Swahili Studies**
eajss.eanso.org
**Volume 6, Issue 1, 2023**
**Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475**
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Utathmini wa Maudhui katika Nyimbo Teule za Newton Kariuki

*John Muriuki Ireri[1*] na Dkt. Onesmus Ntiba, PhD[2]*

[1] Chuo Kikuu cha Mount Kenya, S. L. P. 342-01000, Thika, Kenya.
[2] Chuo Kikuu cha Chuka, S. L. P. 109-60400, Chuka, Kenya.
[*] ORCID ID: https://orcid.org/0000-0002-0632-7368; Barua pepe ya mawasiliano: johnmuriukiireri@yahoo.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1419**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*09 Septemba 2023*

**Istilahi Muhimu**:

*Nyimbo, Maudhui, Mtindo, Newton Kariuki, Umtindo na Udenguzi.*

**IKISIRI**

Makala hii inahusu utathmini wa maudhui katika nyimbo teule za msanii Newton Kariuki. Nyimbo ni moja wapo ya njia zinazotumiwa na wasanii kuwaslisha ujumbe unaowahusu jamii. Utafiti huu ulitumia nadharia ya mseto, yaani nadharia ya umtindo ile ya udenguzi. Nadharia ya umtindo inasisitiza kuwa lugha ina sehemu mbili zinazodhihirika katika usemaji; lugha ni dhahiri na dhahania. Aidha, nadharia ya udenguzi huashiria mgogoro usiosuluhika uliopa baina ya usemi balagha na mawazo kwamba kuna pengo kati ya inachokusudia kusema kazi ya fasihi na inacholazimika au kuelekezwa kusema. Hivyo kuna mvuto katika ya usemi na mantiki. Utafiti ulichukua muundo wa kimaelezo. Mtafiti aliteua kimakusudi jumla ya nyimbo kumi zilizoimbwa na mwanamuziki Newton Kariuki, yaani tano za Kiswahili na tano za Kimbeere. Kutokana na jumla ya nyimbo hamsini alizokuwa ameimba kufikia muda wa kufanya utafiti. Data ilikusanywa kwa kuzingatia kigezo cha yaliyomo. Waaidha, data ilichanganuliwa na kuwasilishwa kwa njia ya kimaelezo. Matokeo ya utafiti ni kuwa sampuli iliyoteuliwa ilisheheni maudhui ya mapenzi, ndoa na familia, migogoro katika ndoa, kuporomoka kwa maadili, uongozi na siasa, umaskini, uhalifu, mawaidha, UKIMWI na dini na imani. Maudhui haya yaliakisi maisha katika ulimwengu wa kiuhalisia. Umuhimu wa makala hii ni kuwa matokeo haya yanadhihirisha kuwa mwimbaji yeyote halengi tu kuburudisha bali kuelimisha. Hivyo makala hii inapendekeza utafiti wa baadae ufanywe kwa kuzingatia mahusiano ya uwezo wa kiuana katika sampuli teule.

**APA CITATION**

Melly, J. M., & Ntiba, O. (2023). Utathmini wa Maudhui katika Nyimbo Teule za Newton Kariuki *East African Journal of Swahili Studies*, *6*(1), 319-338. https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1419.

 | This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

**CHICAGO CITATION**

Ireri, John Muriuki and Onesmus Ntiba. 2023. "Utathmini wa Maudhui katika Nyimbo Teule za Newton Kariuki". *East African Journal of Swahili Studies* 6 (1), 319-338. https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1419.

**HARVARD CITATION**

Melly, J. M., & Ntiba, O. (2023) "Utathmini wa Maudhui katika Nyimbo Teule za Newton Kariuki", *East African Journal of Swahili Studies*, 6(1), pp. 319-338. doi: 10.37284/jammk.6.1.1419.

**IEEE CITATION**

J. M., Ireri, & O., Ntiba "Utathmini wa Maudhui katika Nyimbo Teule za Newton Kariuki", *EAJSS*, vol. 6, no. 1, pp. 319-338, Sep. 2023.

**MLA CITATION**

Ireri, John Muriuki & Onesmus Ntiba. " Utathmini wa Maudhui katika Nyimbo Teule za Newton Kariuki ". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 6, no. 1, Sep. 2023, pp. 319-338, doi:10.37284/jammk.6.1.1419.

## UTANGULIZI

Kulingana na Wamitilia (2004), fasihi ni sanaa inayotumia lugha na ambayo hujishughulisha na binadamu pamoja na maisha yake na huathiri, hugusa au huacha athari fulani na hupatikana katika umbo ambalo linatambuliwa na jamii fulani. Kutokana na fasili hii, mwandishi huyo anabainisha vipengele vitatu katika kufafanua fasihi, yaani sanaa, lugha na maudhui. Fasihi simulizi una vipera vipana vinne, yaani hadithi/simulizi, maigizo, ushairi simulizi na semi au tanzu banifu. Vijipera vingine vyote vya fasihi simulizi huingia katika vipera hivyo. Nyimbo, kwa mfano, ni mfano kijipera cha kipera cha ushairi simulizi (Wamitilia, 2004). Mapitio ya maandishi yalibainisha pengo lililopo katika fasihi simulizi hasa katika kipera cha nyimbo.

Kwa mujibu wa Kamusi ya Karne ya 21 (2013), nyimbo ni maneno na sauti zilizopangwa kama ngoma ambazo huwa ni muziki, sauti zilizopangwa kimuziki. Wamitilia (2004) anakuli kuwa nyimbo ni tungo zenye mahadhi ya sauti inayopanda na kushuka, zinazoundwa kwa lugha ya mkato, matumizi ya picha na mapigo ya silabi. Sanaa hii ya nyimbo hupitisha jumbe mbalimbali kwa hadhira. Hisia za mtu pamoja na dhamira yake humwezesha kuimba nyimbo ambazo hulingana na mawazo yanayoibuliwa akilini mwake. Mawazo haya huwasilishwa kwa hadhira kupitia nyimbo ambazo huwa na maudhui mbalimbali kutegemea kile msanii anataka kukiwasilisha kwa hadhira yake. Masuala yanayowaathiri wanajamii katika mazingira ya msanii huweza kumpa msukumo wa kutunga na kuimba nyimbo ili kuyaweka wazi masuala hayo. Makala hii iliangazia nyimbo za mwimbaji Newton Kariuki ambaye huimba nyimbo zake katika lugha ya Kimbeere na Kiswahili.

Msanii Newton Kariuki huimba nyimbo pendwa ambazo huyasawiri masuala anuwai katika jamii. Kufikia wakati wa utafiti huu, mwimbaji huyu alikuwa ameimba nyimbo sana kwa lugha yake ya mama na lugha ya Kiswahili. Hata hivyo, utafiti huu ulilenga kuchanganua maudhui na mtindo katika nyimbo kumi teule za msanii huyu, tano alizoziimba kwa lugha ya Kimbeere na tano alizoziimba kwa lugha ya Kiswahili. wasomi na watafiti wengi wameshughulikia vipengele mbalimbali katika nyimbo za wasanii mbalimbali. Hata hivyo, kufikia wakati tulipouanza utafiti wetu, hakuna utafiti wowote uliokuwa umefanywa kuhusu maudhui na mtindo wa nyimbo za msanii Newton Kariuki, jambo ambalo utafiti huu umefanya. Msanii Newton Kariuki ni miongoni mwa wasanii wa nyimbo za kizazi kipya ambacho kinatumia lugha ya kiasili kuwasilisha jumbe ambazo zimesheheni mafunzo mengi kwa wanajamii wao. Nyimbo za Newton Kariuki zimeibuka kuwa pendwa na zinawavutia wanajamii wa Mbeere na kwingineko katika janibu hizi.

## MAPITIO YA MAANDISHI

Mutwiri (2005) alitafiti kuhusu mitazamo ya utendakazi wa nyiso katika jamii ya Watigania ambao ni jamii ya watu katika jamii pana ya Wameru. Utafiti wake ulishughulikia majukumu au maudhui ya nyimbo hizo za nyiso. Utafiti huu

ulibainisha kuna ukuruba wa karibu sana kati ya lugha na muktadha wa jamii. Utafiti huu ulitufaa sana hasa katika kukiangazia kipengele cha lugha katika nyimbo teule.

Simiyu (2007) alifanya utafiti kuhusu maudhui na lugha katika nyiso za Wabukusu. Anaeleza kuwa nyimbo hutegemea jinsi wakati unavyobadili maudhui na lugha. Utafiti wake ulitufaa kuelewa jinsi masuala yaliyoibuliwa na msanii Newton Kariuki, pamoja na mbinu alizozitumia zilivyobadilika kiwakati.

Mbogo (2008) alitafiti kuhusu nyimbo za harusi katika jamii ya Waembu. Utafiti wake ulionyesha kuwa maudhui ya nyimbo hizo yalibadilika kiwakati. Kazi hii itatusaidia kuelewa mabadiliko ya maudhui katika nyimbo za Newton Kariuki tulizozichanganua.

## MISINGI YA NADHARIA

Makala hii ilitumia nadharia ya mseto ambazo ni nadharia ya udenguzi na ile ya umtindo. Nadharia ya umtindo iliasisiwa na mwanaisimu Buffon mnamo mwaka wa 1930. Kulingana na mwanaisimu huyu, mtindo ni namna msanii anavyoitumia lugha ili kupitisha ujumbe wake kwa hadhira. Saussure (1983) anadai kuwa lugha ina sehemu mbili zinazodhihirika katika usemaji yaani, lugha dhahiri na lugha dhahania. Utafiti huu walenga kuchunguza msanii Kariuki anatumia mtindo gani. Ni lugha dhahiri au ni lugha isiyo na asili yake. Crystal na Davy (1969) katika mtazamo wao wanasema kuwa lengo kuu la umtindo ni kuziweka wazi fani mbalimbali ambazo anazitumia kuwasilisha maudhui katika kazi yake. Kauli hii ilifaa utafiti huu kwa kuzingatia sifa kuu zinazopatikana katika nyimbo za msanii Kariuki.

Udenguzi ni nadharia iliyotokana na Mfaransa Jacques Derrida. Kulingana na mwasisi huyu, 'neno huendelea kuahirisha maana yake ya mwisho jambo linaloifanya maana kukosa utangamano' (Wafula na Njogu, 2007). Nadharia hii ilitumika kurejelea nadharia ya karne ya ishirini inayotazama mabadiliko na hali inayomfanya msomi kuumbua muundo wa maandishi au kazi ya fasihi. Baada ya kuumbua maandishi, msomi anapata maana kulingana na ung'amuzi au tajriba ya jamii yake. Kulingana na Wafula na Njogu (2007), nadharia ya udenguzi ni miongoni mwa nadharia zinazopuuza mihimili ya kimapokeo kuhusu kazi za fasihi. Nadharia ya udenguzi inaashiria mgogoro usiosuluhika uliopo baina ya usemi balagha na mawazo kwamba kuna pengo kati ya kinachokusudia kusema kazi ya fasihi na kinacholazimika au kuelekezwa kusema. Hivyo, kuna mvuto kati ya usemi na mantiki.

Kwa mujibu wa Derrida (1973), mvutano baina ya vinyume daima huzusha kovu lisilofutika. Wadenguzi hudai kwamba daima kuna mvutano baina ya "kuwepo na kutokuwepo" na maana kuibainisha kutokana na matini. Katika kovu hilo, udenguzi ni mkabala unaolenga katika kuingilia matini kati, kuihakiki ndani kwa kuipeperusha, kuipindapinda na kuonyesha uwezekano wa kutokuwa na vidato vya kinyume (kama ilivyopendekezwa na Saussure). Wanadai kwamba kwenye kinyume ndiko kwenye maingiliano. Udenguzi ni kile kinachotokea katika maana wakati lugha inaeleweka kama maandishi. Maana ya lugha hiyo haitokani na dhana ya mtumiaji wa lugha binafsi kwa sababu dhana tayari zinatendeka katika lugha isiyotokana na dhana hizo.

## MBINU ZA UTAFITI

Mweteri (2021) akimnukuu Kothari (2004) anasema kuwa muundo wa utafiti unajumuisha dhana mbalimblai kama vile nini, wapi, lini, kwa kiasi gani na kwa namna gani kuhusu suala la utafiti. Utafiti huu umechanganua maudhui na mtindo wa nyimbo kumi teule za msanii Newton Kariuki. Utafiti huu ulifanywa nyanjani kwani ulihusu kusikiliza nyimbo teule na kuzinukuu moja kwa moja.

Utafiti huu ulifanywa katika kaunti ndogo ya Mbeere Kaskazini katika kaunti ya Embu. Hili ndilo eneo alikozaliwa na kulelewa msanii Newton Kariuki. Eneo hilo pia lina wengi wa mashabiki wa msanii

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1419

huu. Sehemu ya utafiti huu pia ilifanyiwa maktabani kwani mtafiti alilazimika kusoma vitabu na tafiti mbalimbali zinazohusiana na utafiti huu.

Mugenda na Mugenda (1999) wanapendekeza uteuzi wa makusudi katika kuibua data ya utafiti kwa kuzingatia madhumuni ya utafiti. Kwa hivyo, uteuzi wa makusudi wa sampuli ulizingatiwa ili kupata data faafu katika utafiti huu. Nyimbo kumi (tano za Kiswahili na tano za Kimbeere) ziliteuliwa kati ya takribani nyimbo hamsini alizoziimba. Nyimbo za Kimbeere zimenukuliwa na kutafsiriwa. Hizo ndizo nyimbo mtafiti alihisi zingefanikisha utafiti huu. Sababu kuu ya kuchagua nyimbo tano za Kimbeere na tano za Kiswahili sio kuzilinganisha bali ni kupata hoja zaidi. Nyimbo za Kiswahili zina mitindo inayoeleweka moja kwa moja tofauti na nyimbo za Kimbeere ambazo zinamlazimu mtafiti afikirie kwa kina. Matokeo ya makala hii iliwasilishwa kwa njia ya kimaelezo.

## MATOKEO YA UTAFITI

Njogu na Chimerah (1999) wanasema kuwa maudhui ni mawazo ya jumla au mawazo mapana ambayo huwasilishwa katika wakati maalum katika kazi ya fasihi. Kwa kifupi, maudhui ni masuala yanayoangaziwa na msanii katika kazi ya fasihi. Yafuatayo ni baadhi ya maudhui kutokana na nyimbo teule za Newton Kariuki.

### Mapenzi

Katika nyimbo tulizozichanganua, mwimbaji Newton Kariuki alilipa suala la mapenzi uzito sana. Aliyasawiri mapenzi ya aina mbalimbali kama vile baina ya wanandoa, wachumba na vijana. Hebu tutazame baadhi ya nyimbo zilivyoyasawiri mapenzi. Katika wimbo *Muthoni Kifagio*, msanii Kariuki amejitumia mwenyewe kama mhusika aliyekuwa na mpenzi aliyeitwa Muthoni. Katika wimbo huu, hata kama anahisi kusalitiwa na mpenziwe, maneno anayoyatumia yanaonyesha kuwa alikuwa anampenda sana. Katika stanza ya kwanza ya wimbo huu anasema:

*Muthoni nikiku-remember K.K. natoka jasho*

*Muthoni nikikuremember natiririkwa na machozi*

Katika stanza ya tatu, KK anaeleza jinsi Muthoni alivyokuwa amekonda wakati walipokutana. Isipokuwa mapenzi, hakuna kingine kingemfanya Kariuki kumkubali Muthoni katika hali anayoisawiri. Hebu tazama maneno ya stanza hii.

*If I can remember the day tulionana na wewe*

*Ulikuwa very thin and worn out if I remember*

*Sidhani kama kuna mwanaume angekufikiria*

*Na mimi nikakulisha mpaka ukamea madiaba*

Katika stanza ya kwanza ya wimbo *Kiumbu ni gikuu (Mapenzi ni kifo)*, Kariuki anasema jinsi alivyotoka kwao Gachoka akamwita rafikiye Gacinga ampleke akamwone mpenziwe kwa kuwa mapenzi yalikuwa mengi. Hebu tazama michororo hii ya stanza hiyo ya kwanza.

| Asilia | Tafsiri |
|---|---|
| *Naumire gwetu Gachoka* | Nilitoka kwetu Gachoka |
| *Ngithii ngioca Gacinga* | Nikamwita Gacinga anipeleke |
| *Navetwe 'date' ni mwiritu* | Nilikuwa naenda kumwona mpenzi |
| *Yarigicene ta mutura* | Mapenzi yalikunjana kama nyama ya mtura |

Katika stanza ya tatu ya wimbo huo, msanii anamtaja mpenziwe kama msichana mrembo kama runinga. Hata kama mamake msichana huyo hataki msanii awe na uhusiano wa kimapenzi na binti yake kwa kuwa anamwona msanii kama kizee kikongwe, msanii hakati tamaa. Hebu itazame stanza ifuatayo.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1419

| Asilia | Tafsiri |
|---|---|
| *Mucungwa mwaro ta TV* | Msichana mzuri kama runinga |
| *Mucungwa mwaro ta TV* | Msichana mzuri kama runinga |
| *Nonire ng'ina aukite agitetaga* | Nilimsikia mamaye akiteta |
| *Netirwe ithuri ikuru* | Akaniita kizee kikongwe |
| *Ni mwari ngwenda kwananga* | Eti nataka kumwaribia bintiye |
| *Ndakandeterere mwengeu* | Sitaki kuletewa kisirani |

Katika stanza ya mwisho ya wimbo huo, msanii anaapa kwamba ifikapo Disemba atafika mapema sana ili amwone mpenziwe. Hata ingawa mamake mpenziwe hamtaki msanii, anajikumbusha ukweli wa methali kuwa dua la kuku halimzuii mwewe kumchukua kifaranga. Hii inamaanisha ameapa kuwa hata ingawa atahatarisha maisha yake hakuwa tayari kumwacha msichana huyo. Ni mapenzi tu yanayoweza kumfanya mtu kufanya uamuzi kama huo. Hebu tazama maneno haya

| Asilia | Tafsiri |
|---|---|
| *Disemba nwambaka nthame kuo* | Nitaenda huko Desemba |
| *Thaa imwe ikirungama ngakorwa vau* | Nitafika saa moja |
| *Ninanyitire ndeto na FM* | Nimepata habari na FM |
| *Nyama noru ta ngurwe* | Nyama nono kama ya nguruwe |
| *Ndiu nditigaga gacui* | Mwewe hamwachi kifaranga |
| *Nundu wa kirumi kia nguku* | Kwa sababu ya dua la kuku |

**Ndoa na Familia**

Kulingana na *Kamusi ya Kiswahili Sanifu toleo la 4*, ndoa ni makubaliano rasmi baina ya mwanamke na mwanamume kuishi pamoja kama mume na mke. Katika miktadha mbalimbali ya kijamii, mwanamume na mwanamke wanaweza kukubaliana kuishi pamoja kama mume na mke hata ingawa hakuna urasmi wowote. Hali kama hizi zote hukubaliwa kama ndoa baina yao. Ndoa huzaa familia na hivyo, katika kuangalia maudhui haya, familia ni kiungo muhimu cha ndoa. Msanii Kariuki amezungumzia sana suala la ndoa na familia katika nyimbo tulizozichanganua. Hebu tuangalia mifano ifuatayo.

Katika wimbo *Ng'ombe irikite nyomba (Ng'ombe ameingia ndani ya nyumba)*, msanii ameisawiri ndoa ambapo anaonyesha mfano wa sababu za familia kuvunjika. Katika stanza ya kwanza ya wimbo huu anamtaja mwanamke anayelia kwa kuwa mumewe alikuwa 'amemchukua' bintiye. Hii inamaanisha kuwa baba alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na mtoto wake. Mkewe analia kwani kitendo hicho kilikuwa kinaenda kinyume na msingi wa familia na ndoa na kilikuwa hatari kwa usalama wa ndoa yake. Hebu tazama mishororo hii kutoka stanza hiyo.

| Asilia | Tafsiri |
|---|---|
| *Nethire mwongia akiugaga mbu uui uuii* | Nilimkuta mwanamke akilia uui uuii |
| *Ukani mwone ii muthuri ii* | Njooni mwone baba |
| *Egwoca mwari* | Amemchukua bintiye |

Katika stanza ya pili ya wimbo huo tunamwona mzee anayesemekana anamchukua mkaza mwana na kumfanya bibi yake. Hali kama hii ni tishio kwa ndoa mbili, ile yake na ya mwanawe. Hebu tazama mishororo ifuatayo ya stanza hiyo.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1419

| Asilia | Tafsiri |
|---|---|
| *Mavitia mama ni ma avava aria matuciarire* | Makosa ni ya kina baba wazazi wetu |
| *Mavitia mama ni ma avava aria matuciarire* | Makosa ni ya kina baba wazazi wetu |
| *Muka wa mwana ndakarikia aramwoca* | Anamchukua mkaza mwana kuwa bibi yake ta wake |

Katika wimbo *Kuuma wauma gwakwa (Tangu ulipotoka kwangu)*, msanii Kariuki anaonyesha watu waliokuwa wameoana lakini wakaachana. Pasona katika wimbo huu anasema kuwa imepita miaka mitatu tangu mwanamke alipotoka kwake. Kulingana naye, hakuwa na chuki na mwanamke yule. Hebu tazama stanza hii ya kwanza ya wimbo huo.

| Asilia | Tafsiri |
|---|---|
| *Kuuma wauma gwakwa ni miaka ithatu* | Tangu ulipotoka kwangu ni miaka mitatu sasa |
| *Kuuma wauma gwakwa ni miaka ithatu* | Tangu ulipotoka kwangu ni miaka mitatu sasa |
| *Wathiire na ndwanaivugura* | Ulienda bila kuangalia nyuma |
| *Nii ninekire ciindu* | Mimi nimetajirika |
| *Nii ndiakumenete* | Sikuwa na chuki nawe |

Katika stanza ya pili ya wimbo huu, mume aliyeachwa na mkewe anasikika akimwambia mke huyo iwapo atapata nafasi aende akawaone watoto wake aliowaacha. Inaonekana, kwa sababu ya mapenzi ya watoto wake, anataka mama yao arudi nyumbani angalao awajulie hali. Pia, katika stanza iyo hiyo anamwambia mwanamke huyo kuwa alipomwacha, alishindwa kuishi peke yake hivyo alioa mke mwingine. Hebu tazama mishororo ifuatayo kutoka kwa stanza hiyo.

| Asilia | Tafsiri |
|---|---|
| *Wagia na kavinda cuthagira ciana* | Ukipata nafasi uje uwaone watoto wako |
| *Wathii ninavikanirie, U-single niwanemire* | Ulipoenda nilishindwa kukaa pekee nikaoa tena |
| *Riu mucii urina mwene* | Sasa boma lina mwenyewe |

Katika stanza ya mwisho, tunamsikia mwanamume katika wimbo huo akimwambia mke aliyemtoroka arudi nyumbani aajiriwe na mke mwenza kuwinda wanyama aina ya kuchakulo. Hata ingawa anamkejeli hapa, suala la ndoa linajitokeza vilivyo. Tazama mshororo ufuatao wa stanza hiyo.

| Asilia | Tafsiri |
|---|---|
| *Coka urirage nduru wandikwe ni mwiruguo* | Rudi uajiriwe na mke mwenza kuwinda kuchakulo |

Katika wimbo *Muthoni kifagio*, msanii anakumbuka jinsi alivyokuwa anaishi na Muthoni kwake na kumfanyia kila kitu mwanamume anapaswa kumfanyia mwanamke. Hata hivyo anahuzunika sana kuwa pamoja na hayo yote Muthoni alimsaliti na kumwacha. Inaonekana lilikuwa lengo la KK kuishi na Muthoni katika ndoa. Hebu tazama mishororo ifuatayo ya stanza ya kwanza ya wimbo huo.

*Muthoni nikiku-remember KK natoka jasho*

*Muthoni nikikuremember natiririkwa na machozi*

*Nikikumbuka vile nilikuwa nimeku-keep kwangu*

Katika wimbo *Mke ni bahati*, msanii Kariuki anazungumzia ndoa. Mwimbaji anaeleza sifa za mke mzuri katika ndoa kulingana na mawaidha ya babu yake. Katika stanza ya kwanza, anasema kuwa kulingana na babu yake, mke mzuri ni yule anayefuata amri zako katika ndoa. Hebu tazama stanza hii ya kwanza.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1419

*Babu aliniambia hakuna mke mzuri*

*Mwanamke mzuri ni yule ukimwoa*

*Anafuata amri zako kama wa Israeli na Musa*

Katika stanza ya tatu ya wimbo uo huo, mwimbaji anaonyesha kuwa watu huoana kupitia harusi makanisani. Hebu tazama mshororo huu wa kwanza wa stanza hiyo.

*Wengi mnooa kwa harusi makanisani*

Katika stanza ya sita, mwimbaji anawakumbusha wanaume kuwa walipooa waliapa kuishi na wake zao hadi milele na hivyo wanapaswa kuvumilia maisha katika ndoa hata kama wanateseka. Hebu tazama maneno ya stanza hiyo.

*Kumbuka uliapa utaishi na yeye milele*

*Sasa amekwisha breki*

*Brother vumilia upelekwe mbio kama magari ya miraa*

Katika stanza ya saba ya wimbo huo, mwimbaji anawakumbusha wanaume wanaoteseka katika ndoa kuwa hata yeye na wengine waliowaoa wake wazuri hawakubahatika bali wamechangia kwa wake wao kuwa na tabia nzuri. Tazama stanza hiyo hapa.

*Ndugu usifikiri sisi tulibahatika*

*Tukaoa wazuri*

*Wale tunao nyumbani*

*Wengi ni recondition kama magari ya Dubai ii*

Katika stanza ya mwisho ya wimbo huu, mwimbaji anawaeleza wanaume kile wanachostahili kufanya ili waweze kuishi vyema na wake wao katika ndoa. Hebu tazama maneno ya stanza hiyo hapa.

*Kwa hivyo ukioa usifikiri umefaulu*

*Lazima ubomoe engine*

*Yaani tabia zake*

*Uweke ring mpya*

*Ndio mpate kuishi iii*

Katika wimbo *Safari ya Meru,* msanii Kariuki anawataja wasichana Wameru kuwa wamesoma na wenye nidhamu. Anasema kuwa ni watu wanaojua kutunza ndoa kwani ukimwoa msichana Mmeru unapewa guarantee ya miaka kumi ya kuishi naye bila kukosana. Anawaambia marafiki wake waoe wasichana wameru. Tazama mishororo ifuatayo ya stanza ya mwisho ya wimbo huo.

*Wasichana wa huko Meru*

*Ni wasichana wamesoma wenye nidhamu*

*Nilipata kujua ukioa Mmeru*

*Unapewa guarantee ya miaka kumi*

*Ya kuishi na huyo bibi huyo bila kukosana Ya kuishi na huyo bibi huyo bila kukosana*

*Wamboni, oa Meru*

*Wamboni, oa Meru*

*Onesi oa Meru*

*Onesi oa Meru*

*Wakasioki oa Meru*

*Simba mundu oa Meru*

*Simba mundu oa Meru*

*Upewe guarantee ya miaka ishirini ya kuishi na huyo bibi kweli bila kukosana maisha aaa*

**Migogoro katika Ndoa**

Kwa kawaida watu wawili hawawezi kuishi pamoja bila kuwa na mitazamo au misimamo tofauti. Vivyo

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1419

hivyo kwa wanandoa. Mara nyingine huwa na kutoelewana katika ndoa ambayo isiposhughulikiwa mapema huenda ikaisambaratisha ndoa husika. Msanii Newton Kariuki ameonyesha kuwa ndoa na familia huwa na changamoto ambazo mara nyingi watu wa nje hawawezi kuzitambua. Hebu tuone jinsi alivyoyasawiri maudhui hayo katika baadhi ya nyimbo tulizoziteua.

Katika wimbo *Murivua ni muka (Anayepigwa na mkewe)*, msanii Newton Kariuki amesawiri hali ambapo wanandoa wanapigana. Vita kati ya wanandoa ni baadhi ya matatizo yanayozikumba familia. Katika stanza ya kwanza ya wimbo huu anauliza swali balagha, yaani anayepigwa na mkewe hujificha wapi? Kwa namna fulani msanii huyu anatuambia kuwa hata ingawa si jambo la kawaida, wanaume wengine hupigwa na wake wao. Hebu tazama stanza hii.

| **Asilia** | **Tafsiri** |
|---|---|
| *Murivua ni muka auraga nevenya* | Anayepigwa na mkewe hukimbia mbio |
| *Murivua ni muka auraga nevenya Murivirwa gwake ethithaga ku?* | Anayepigwa na mkewe hukimbia mbio<br>Anayepigwa na mkewe hujificha wapi? Labda jikoni kwa mama yake |
| *Twangana garuri ya nina* | |
| *Ndikwona vena "otherwise"* | Sioni pakiwa na njia nyingine |

Katika stanza ya pili ya wimbo huo, mwimbaji anachora taswira kuwa si ajabu kwa mke kupigwa na mumewe kwani hata hili likifanyika mke ataenda nyumbani tu. Hebu tazama mishororo ifuatayo ya stanza hiyo.

| **Asilia** | **Tafsiri** |
|---|---|
| *Muriva muka muka enukaga wa mucii* | Anayempiga bibi yake bibi huenda nyumbani |
| *Muriva muka muka enukaga wa mucii* | Anayempiga bibi yake bibi huenda nyumbani |

Katika stanza ya tano, mwimbaji anasema kuwa ni vigumu kujua kuwa wanaume huchapwa na wake zao. Hii ni kwa sababu kule nje wanaume hao wamejaa ukakamavu. Amefananisha sauti zao kule nje kama ngoi wa usiku. Wanaume hawa huwa wakali wakiwa nje lakini wakifika nyumbani wanatulia na kuwa wororo kama chapati na ni Mungu tu humhurumia kwani mkewe hana huruma naye. Hebu tazama stanza hiyo.

| **Asilia** | **Tafsiri** |
|---|---|
| *Murivua ni muka ungimwithira arumeri* | Anayetandikwa na mkewe ukimkuta nje |
| *Murivua ni muka ungimwithira arumeri* | Anayetandikwa na mkewe ukimkuta nje |
| *Ndugecirie ungithii wokimumenya* | Usifikiri utamtambua mara moja |
| *E kanua kanene nita ngui ya utuku* | Ana sauti kubwa kama ngoi wa usiku |
| *Nginya vinya onekaga arwa nayo* | Anaonekana mwenye nguvu |
| *Ndungimuvuthia mukarega kurua Na angithii* | Ukimdharau mtapigana |
| *kwi muka atemagwa ni kaveni* | Na akienda nyumbani anakuwa na wasiwasi sana |
| *Agitota ta cavati* | Anakuwa mwororo kama chapati |
| *Ni Ngai iriraga nantha* | Ni Mungu humhurumia |

Katika stanza ya sita, mwimbaji anasema kuwa yeye hawezi kuchapwa na mke aliyemwoa. Anaongeza kuwa hata afadhali mke huyo amuue kabisa. Hii bila shaka inaonyesha kuwa kuna wanaume wanachapwa na wake zao jambo ambalo linachangia kutokuwa na amani katika familia. Hebu tazama mishororo ifuatayo ya stanza hiyo.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

| Asilia | Tafsiri |
|---|---|
| *Mundu muka ngurite ndiitikitie nwandive* | Mimi siwezi pigwa na bibi yangu |
| *Mundu muka ngurite ndiitikitie nwandive* | Mimi siwezi pigwa na bibi yangu |
| *Wana eci karate nikava ngakwira vo…* | Hata kama anajua karate afadhali aniue |

Katika wimbo *Kiumbu ni gikuu (Mapenzi ni kifo)*, msanii Kariuki anatuwasilishia mama mmoja ambaye alifukuzwa na mumewe na siku hizi anaishi katika kambi ya chifu. Ili mama huyu afukuzwe katika ndoa yake bila shaka kulikuwa na tatizo kati yake na mumewe au familia ya mumewe. Hebu tazama mishororo ifuatayo kutoka stanza ya pili ya wimbo huo.

| Asilia | Tafsiri |
|---|---|
| *Niwengatirwe ni murume* | Alifukuzwa na mumewe |
| *Araraga kambi karambari* | Siku hizi hulala kambi ya chifu |

Katika wimbo *Ngoma bila nguo*, msanii anatuonyesha kuwa moja kati ya mambo yanayoweza kuleta shida katika ndoa au familia ni uasherati. Mwimbaji na wenzake wanapovamiwa na wezi na kuamrishwa wavue nguo zao, baadaye walivaa nguo zozote walizozipata na kuenda nyumbani. Anasema kuwa alipofika nyumbani, moja kati ya nguo alizozivaa ilikuwa ya kike na ilikuwa na harufu ya marashi. Hapa anatueleza kuwa mkewe alikuwa ameleta shida sana kwani alifikiri kuwa mwimbaji alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na mwanamke mwingine. Anasema kuwa iwapo yeye alipata shida vile bila shaka yule mzee waliyekuwa naye kwenye ngoma na akavaa *biker* ambayo ni nguo ya ndani ya wanawake bila shaka alipata shida kubwa sana kutoka kwa mkewe. Hebu tazama stanza zifuatazo za wimbo huo.

*Yule mzee alikuwa na kitambi*

*Alitafuta nguo ya kuvaa akakosa*

*Mwishowe alivaa biker*

*Ilikuwa imebaki bila mwenyewe*

*Hakuna mtu alipata nguo yake*

*Kama mimi zile nilivaa*

*Nilipofika kwa nyumba yangu*

*Moja yazo haikuwa ya mwanaume*

*Hako kanguo kangefanya tukosane Na bibi yangu mama watoto*

*Hako kanguo kangefanya tukosane*

*Na bibi yangu mama watoto*

*Alikuwa ameleta shida sana*

*Kwa sababu kananuka marashi*

*Na akasema niwache kum-enjoy Ujanja wangu umefika mwisho*

*Nafikiria mwenye kuvaa biker Alikuwa na shida kuliko mimi*

*Nafikiria mwenye kuvaa biker*

*Kwa bibi yake alipata shida sana*

**Kuporomoka kwa Maadili**

Kulingana na *Kamusi ya Kiswahili Sanifu toleo la 4*, maadili ni mwenendo mwema. Kila jamii huwa na vigezo vinavyoongoza wanavyoishi na kuweka mipaka kati ya yale yanayokubalika na yale yasiyokubalika katika jamii husika. Katika nyimbo tulizoziteua, msanii Newton Kariuki ameonyesha wahusika mbalimbali ambao kulingana na anavyowasawiri, wameenda kinyume na maadili. Hebu tuone baadhi ya nyimbo zinazoyasawiri maudhui ya kuporomoka kwa maadili.

Katika wimbo *Ng'ombe irikite nyomba (Ng'ombe ameingia ndani ya nyumba)*, tunamwona mzee ambaye anakosa adabu na kuwa na urafiki wa kimapenzi na bintiye. Hebu tazama mishororo hii ya stanza ya kwanza ya wimbo huo.

| **Asilia** | **Tafsiri** |
|---|---|
| *Ukani mwone ii muthuri ii* | Njooni mwone baba |
| *Egwoca mwari* | Amemchukua bintiye |

Katika stanza ya pili ya wimbo huo, mwimbaji anatuambia kuwa familia nyingi zinavunjika kwa sababu za tabia za kina baba. Anatupa mfano wa baba ambaye anamchukua mkaza mwana na kumfanya mkewe. Hakika huu ni ukosefu wa maadili kwani mkaza mwana wake ni kama binti yake. Pia, anapomchukua mke wa mwanawe anatarajia mwanawe afanye nini? Hebu tazama mishororo ifuatayo ya stanza hiyo.

| **Asilia** | **Tafsiri** |
|---|---|
| *Riu mukwona micii mingi ikithuka* | Mnapoona boma nyingi zikivunjika |
| *Mavitia mama ni ma avava aria matuciarire* | Makosa ni ya kina baba wazazi wetu |
| *Mavitia mama ni ma avava aria matuciarire* | Makosa ni ya kina baba wazazi wetu |
| *Muka wa mwana ndakarikia aramwoca ta wake* | Anamchukua mkaza mwana kuwa bibi yake |

Katika stanza hiyo ya pili, mwimbaji anatuambia kuwa wasichana siku hizi wanaenda kinyume cha maadili kwa kuvaa sketi fupi zinazofika magotini ilhali hawavai kamisi. Kulingana na mwimbaji, huu ni ukosefu wa maadili. Inaonekana mwimbaji ametoka katika utamaduni ambapo wasichana walipaswa kuvaa sketi au marinda marefu. Hebu tazamam mishororo hii kutoka katika stanza hiyo.

| **Asilia** | **Tafsiri** |
|---|---|
| *Nario rika riria ririkuo riu* | Nao rika liliko siku hizi |
| *Tabia ni mboru* | Tabia ni bovu |
| *Cikati ni nguvi ya maru* | Sketi fupi za magotini |
| *Na ndari kamithi* | Na hawavai kamisi |

Katika stanza ya pili pia, mwimbaji anatuambia kuwa siku moja aliona maajabu ya mzee kumtongoza bintiye. Anasema kuwa huyo mzee hakuwa na aibu. Pia anamuuliza mzee huyo ni kwa nini anamtongoza binti yake. Ingekuwa kitendo hiki kilikubalika katika jamii hiyo, mwimbaji asingesema mzee huyo alikosa adabu. Hebu tazama mishororo ifuatayo kutoka stanza hiyo.

| **Asilia** | **Tafsiri** |
|---|---|
| *Nakinya Meka nethire uriru* | Nilipofika Meka niliona maajabu |
| *Muthuri egwitia mwari uriru  Muthuri nindui ugwitia mwariguo ukinungaga ukuru* | Mzee  anamtongoza bintiye |
| *Muthuri nindui ugwitia mwariguo ukinungaga uthuri* | Mzee anamtongoza bintiye Mzee ni nini unamwitisha bintiyo unanuka uzee? |
| *Muthuri nindui ugwitia mwariguo na ndungiconoka* | Mzee ni nini unamwitisha bintiyo ukinuka uzee? |
| *Nindui ugwitia mwariguo?* | Mzee ni nini unamwitisha bintiyo na hata huna aibu? |
| | Mbona unamtongoza bintiyo? |

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1419

Katika stanza ya nne ya wimbo huo, mwimbaji anamtaja mzee aliyemdanganya mkewe kuwa alikuwa anaenda Embu. Naye mkewe akatoka akaenda shughuli zake katika vyama vya kina mama. Baadaye mzee yule anarudi nyumbani na kujaribu kumnajisi bintiye. Kisadfa ikawa mkewe alikuwa amekisahau kibeti cha pesa na hivyo akarudi nyumbani na kumfumania mumewe akitaka kumnajisi bintiye. Huu ni mfano wa kuporomoka kwa maadili katika jamii. Hebu tazama mishororo ifuatayo kutoka stanza hiyo.

| Asilia | Tafsiri |
|---|---|
| *Cira nene nethire Meka iii* | Kesi kubwa nilikuta Meka |
| *Muthuri atigite avenia muka niwathii Embu* | Mzee kamdanganya mkewe ameenda Embu |
| *Nake muka akiumagara akithii nguruvuri cia aka* | Naye mkewe akaenda chama cha kina mama |
| *Muthuri wakinaemirania wagicokerera mwari* | |
| *I wana ruga rugukua ii making'ang'ana* | Mzee kajificha akamrudia bintiye |
| *Nake muka egutiga mbeti wakivanga amiciokere* | Akavuja kibuyu aking'ang'ana naye |
| | Naye mkewe akaamua kurudia pesa alizoziacha |
| *Nake muka egutiga mbia ii wakivanga aicokere* | Ile picha mkewe aliona mimi siwezi kusema |
| *Amwithire uguo ukwenda wee. nari ii nii tingwetekia* | Mkewe kasahau kibeti na akakirudia |

Ili kuthibitisha kuwa alichokifanya mzee huyo katika wimbo huo, vijana katika eneo hilo walifanya maandamano ya amani kukikashifu kitendo cha mzee huyo. Walikuwa wakiuliza iwapo wazee wataendelea kuwachukua wasichana kama hao, wao vijana wangewaoa kina nani? Walisema kuwa wazee kama wale walikuwa wakiwaharibia wachumba wao. Tazama mishororo ifuatayo kutoka stanza ya tano ya wimbo huo.

| Asilia | Tafsiri |
|---|---|
| *Nacio ivici Gachoka ciegua uria muthuri ekire* | Nao wavulana Gachoka waliposikia alivyofanya mzee |
| *Ikiruma mathigi ciike "peaceful demonstration"* | Wakaanza maandamano ya amani |
| *Nugutucukiria aka etu notari namuka? Thui tukagurana ku?"* | Anatuharibia wachumba wetu kwani yeye hana bibi? Sisi tutaoa nani? |

Katika wimbo *Muthoni kifagio*, msanii Kariuki anatuonyesha hali ambapo Muthoni anayasaliti mapenzi ya KK. Usaliti kama huu unaonyesha ukosefu wa maadili. Katika stanza ya pili ya wimbo huu, mwimbaji anasema jinsi alivyomtunza Muthoni kwake Narobi lakini Muthoni alikuwa na tabia mbaya. Tazama mishororo ifuatayo ya stanza hii.

*Maisha ukiwa kwangu ni kama paka dukani*

*Kila siku nyama choma na kadhalika na etcetera*

*Mwishowe niligundua mimi Kari nikienda kazi*

*Unaingia mtaa na route mbaya kama matatu*

Katika stanza ya tano, KK anasema kuwa Muthoni ni teksi bali sio gari la kibinafsi. Jazanda hii inaashiria kuwa Muthoni hakutulia na kutosheka na mapenzi ya KK na kuanza tabia ya kutembea na wanaume wengine, hali ambayo ni kinyume cha maadili katika jamii. Tazama mshororo huu wa stanza hiyo.

*Kumbe wewe ni taxi, sio personal car*

Katika wimbo *Mke ni bahati*, msanii Kariuki anasema kuwa kuna wanawake wanaoolewa ambao hawana tabia nzuri. Katika stanza ya tatu ya wimbo huo, tunaona kuna wanawake wanaolewa hata kupitia harusi kanisani lakini baadaye wanabadilika na kuwa na tabia mbaya. Anasema kuwa wengine wao hata wamewashinda wazazi wao. Tazama stanza hii.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

*Wengi mnaooa kwa harusi makanisani*

*Wameshinda wazazi wao*

*Wengi hawajaokoka*

*Wengi ni vichwa ngumu hata kuliko bibi ya Loti iii*

Katika stanza ya tano, msanii anasema kuwa mwanamke huyo hajali na hata anamtusi mumuwe mbele ya wazazi. Pia ana maringo zaidi ya tausi. Hebu tazama mishororo hii ya stanza hiyo.

*Hajali kukutusi hata mbele ya wazazi*

*Pia anakuringia hata kushinda tausi*

Katika wimbo *Safari ya Meru,* msanii Kariuki anawataja watu ambao wanapenda kueneza uvumi. Walikuwa wameeneza uvumi kuwa mwimbaji Kariuki alikuwa amekufa ilhali ilikuwa uwongo. Kulingana naye, uvumi ni mbaya na watu wanapaswa kuachana nao. Tabia kama hii ni mfano wa ukosefu wa maadili katika jamii. Hebu tazama mishororo ifuatayo kutoka wimbo huo.

*Nikajitambulisha kwa watu wa huko Meru*

*Walikuwa wamepata ripoti ya huzuni*

*Ya kwamba mimi Karish wa Ngari nimekufa*

*Ya kwamba mimi Karish wa Ngari nimekufa na ni uongo Uvumi mbaya, chunga!*

Katika wimbo *Ngoma bila nguo,* tunaona jinsi majambazi wanawavamia watu wakiwa wanajiburudisha na kuwaamrisha wavue nguo. Kulingana na mwimbaji, ukumbi huo wa densi ulijaa watu wa kila rika - wazee, kina mama na wasichana ‘dot com’. Ni ukosefu wa maadili kuwalazimisha watu kama hawa kuvua nguo katika mazingira kama yale. Pia, majambazi wale waliwaibia kila kitu. Watu wanaowafanyia wengine madhila kama haya si watu waadilifu hata kidogo. Hebu tazama mishororo ifuatayo kutoka stanza mbalimbali za wimbo huo.

*Ilikuwa siku ya mateso*

*Ngoma kubwa ilikuwa imejaa*

*Kina mama, wazee na dot com*

*Ilikuwa saa nane ya usiku*

*Nikasikia kila mtu lala chini*

*Tukaamrishwa kila mtu atoe nguo*

*Nguo zetu zote wakakusanya*

*Nawakasema tusonge mbele na ngoma*

*Pesa zetu zote wakabeba*

*Manguo zetu wakatutupia kwa sakafu*

**Uongozi na Siasa**

Msanii Newton Kariuki pia ameyashughulikia maudhui ya uongozi na siasa katika baadhi ya nyimbo zake. Hata hivyo, amefanya hivyo kwa ustadi wa juu kiasi ya kwamba usipokuwa makini hutagundua kuwa anazungumzia siasa na uongozi hasa wa jamii ya Wambeere ambao ni jamii moja katika kaunti ya Embu. Katika siasa za kaunti ya Embu, jamii ya Waembu ni kubwa kuliko ile ya Wambeere na kwa sababu hii, aghalabu viongozi wengi wakubwa wamekuwa wakitoka katika jamii ya Waembu kwa sababu ya wingi wao wa kura. Hebu tuone jinsi msanii Kariuki alivyolisawiri suala la uongozi na siasa.

Katika wimbo *Urathi wina kieva (Utabiri wenye huzuni),* msanii huyu anazungumzia masuala yanayohusu uongozi wa jamii yao. Katika stanza ya kwanza ya wimbo huo anatumia jazanda ya Musa alivyotumwa na Mungu kwenda kuwakomboa wana wa Israeli kutoka Misri. Anasema kuwa Musa alipoambiwa aende alisema kuwa asingeweza lakini Mungu akamwambia kuwa angeandamana na Haruni nduguye. Hata kama kwenda Misri kulikuwa na hatari nyingi, Musa na Haruni walienda. Anasema

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1419

kuwa shughuli hii ilihitaji ujasiri. Jazanda hii inalenga kuwaonyesha viongozi wa jamii ya Wambeere kuwa wanahitaji kufanya kazi kwa pamoja na kuwa na ujasiri iwapo wanataka kuyainua maisha ya watu wao. Hebu tazama stanza hiyo.

| **Asilia** | **Tafsiri** |
|---|---|
| *Musa atumwa ni Ngai agire ciana ukombori* | Musa alitumwa na Mungu aendee watoto utumwani |
| *Musa atumwa ni Ngai agire ciana Misiri* | Musa alitumwa na Mungu aendee watoto Misiri |
| *Agicokeria Ngai nii timbota* | Akamwambia Mungu kuwa hangeweza |
| *Vandu ava varenda mundu uri na kanua karuu* | Hapa panastahili mtu jasiri |
| *Akirwa tanguve Haron agutware* | Akaambiwa apewe Haron waende pamoja |
| *Na nimathiire kunari ugwati* | Walienda hata kama kulikuwa na hatari Walienda |
| *Na nimathiire kunari ugwati Mwigue!* | hata kama kulikuwa na hatari Msikie! |

Katika stanza ya pili ya wimbo huo, msanii anatabiri kuwa wanapoelekea Wambeere wangeanza kulia. Anasema utabiri wake ni wa kweli kwani huwa hasemi mambo ambayo hana uhakika nayo. Katika stanza ya tatu anasema kuwa Mumbeere akiumwa na funza huwa hamtoi bali anasubiri funza huyo afie mwilini. Kwa namna moja au nyingine, msanii anawaonya watu wa jamii yake dhidi ya kutulia tu na kufikiria kuwa mambo yako shwari. Anawataka wajukumike iwapo wanataka kuheshimiwa na kupata nafasi inayostahili katika jamii pana. Hebu tazama stanza hizi.

| **Asilia** | **Tafsiri** |
|---|---|
| *Vau tugiririte ukona Mumbeere akirira* | Mahali tunaelekea utamwona Mumbeere akilia |
| *Vau tugiririte ukona Mumbeere akirira* | Mahali tunaelekea utamwona Mumbeere akilia |
| *Ndirathaga mugio tikwa ndi kavici* | Mimi sifumi upepo kama kijana mdogo Natupa jiwe |
| *Mbikagia ithiga iti mbici rina nyamu* | mahali najua pana mmyama |
| *Mbikagia ithiga iti mbici riri na nyamu ingiriwa* | Natupa jiwe mahali najua pana mmyama anayeweza liwa |

Katika stanza ya nne ya wimbo huo, msanii Kariuki anawaonya wanajamii kuwa miaka hamsini ijayo tangu alipouimba wimbo huo, lugha ya Kimbeere itasahaulika. Anawaasa waanze kuiandika lugha hiyo. Kwa kawaida lugha huweza kusahaulika au kufa iwapo wazungumzaji wake wameacha kuitumia kwa sababu ya kujumlishwa katika utamaduni wa lugha inayotumiwa sana na watu wengi. Msanii huyu anajaribu kuwaeleza wanajamii wake kuwa utamaduni wao umo hatarini iwapo viongozi wao wataketi kitako na kuendelea kuwafuata wengine bila kuuliza maswali. Tazama stanza hiyo hapa.

| **Asilia** | **Tafsiri** |
|---|---|
| *Miaka mirongo itano iguka ndukegua Kimbeere* | Miaka hamsini ijayo hutasikia lugha ya Kimbeere |
| *Miaka mirongo itano iguka ndukegua Kimbeere* | Miaka hamsini ijayo hutasikia lugha ya Kimbeere |
| *Riu ambiririani, gukiandia vandu* | Sasa anzeni kuandika lugha hii mahali |
| *Nimugacaria nyimbo iria Karish ainaga* | Mtatafuta nyimbo zilizoimbwa na Karish |
| *Mumenye Kimbeere, uria kiaragua* | Mjue vile mnapaswa kuongea Kimbeere |
| *Uyu ni urathii uri na kieva* | Huu ni utabiri wenye huzuni |
| *Uyu ni urathii uri na kieva kingi* | Huu ni utabiri wenye huzuni sana |

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1419

Katika stanza ya tano ya wimbo huo, msanii anasema kuwa uchaguzi utakapofika viongozi watachaguliwa kutoka jamii nyingine kama vile Wakamba, Wakikuyu na Watharaka lakini hakutakuwa na Mumbeere kwa kuwa atakuwa tayari ameisha. Huu ni ujumbe mzito sana kwa wanajamii Wambeere na viongozi wao ili wajifikirie kama wanajamii na wajipende inapofika wakati wa uchaguzi ili wawachague pia viongozi miongoni mwao. Ni kwa namna hiyo tu wataweza kuhakikisha jamii yao inaendelea kama jamii nyingine. Hebu tazama stanza hii.

| **Asilia** | ***Tafsiri*** |
|---|---|
| *Kithurano gietua, indi iyo ngugweta* | Uchaguzi ukifikia wakati huo |
| *Kithurano gietua, indi iyo ngugweta* | Uchaguzi ukifikia wakati huo |
| *Gukathurwa Mwikamba kana Mugikuyu* | Kutachaguliwa Mkamba au Mkikuyu |
| *Kana Mutharaka, na ndikuga nai Ti nai tondu Mumbeere agakorwa athirire* | Au Mtharaka na sisemi kwa ubaya Sio vibaya sababu Mumbeere atakuwa ameisha |
| *Uyu ni urathii, uri na kieva* | Huu ni utabiri wenye huzuni |
| *Uyu ni urathii uri na kieva kingi* | Huu ni utabiri wenye huzuni sana |

Katika stanza ya sita ya wimbo huo, msanii Kariuki anachora taswira ya mnyama anayeuma kwa werevu sana hivyo wanaoumwa hawatamwona. Anasema kuwa mnyama huyo anapouma, badala ya kuacha uchungu anaacha mwasho wa aina fulani. Anawaonya wanajamii wake kuwa utamu huwa wa aina tofauti ila utamu huo una huzuni. Anawakumbusha kuwa wana mishale ya kujikinga dhidi ya mnyama huyu lakini hawaitumii mishale hiyo kwani wanaiacha ichomekee nyumbani huku wamesimama na kuanglia tu. Anawakejeli wanajamii kuwa wanangoja moto uzimwe na upepo kwani hawahusiki kwa namna yoyote. Msanii Kariuki anaongea kwa mafumbo hapa. Anawafananisha wale wanaoidhulumu jamii yake kama mnyama anayeuma kwa werevu. Hawa ni watu au jamii ambazo zimekuwa zikifaidika kutokana na jamii ya Wambeere huku wakijionyesha kama marafiki. Anawahimiza wanajamii wachukue hatua wenyewe ili waikomboe jamii yao badala ya kungoja majaaliwa. Hebu tazama stanza hiyo hapa.

| **Asilia** | **Tafsiri** |
|---|---|
| *Nyamu ino ikuruma na wara mutikamiona* | Mnyama huyu anauma kwa werevu hamtamwona |
| *Nyamu ino ikuruma na wara mutikamiona* | Mnyama huyu anauma kwa werevu hamtamwona |
| *Ithenya ria gutiga ururu igatiga mwithua* | Badala ya kuacha uchungu anaacha mwasho |
| *Murio wi mithemba; ava vena kieva Migui nayo nivira nyomba murungii rutere* | Utamu ni tofauti; hapa pana huzuni Mishale nayo yachomekea nyumbani, mkisimama kando |
| *Mweterere mwaki, uvorue ni ruvuvo Mweterere mwaki, uvorue ni ruvuvo Kieva!* | Mnangojea moto uzimwe na upepo<br>Mnangojea moto uzimwe na upepo Huzuni! |

**Umaskini**

Kwa mujibu wa *Kamusi ya Kiswahili Sanifu toleo la 4*, umaskini ni hali ya kukosa mali. Umaskini unaweza kumsababishia mtu kukosa kujitimizia mahitaji ya kimsingi. Msanii Newton Kariuki amelishughulikia suala la umaskini au ukosefu wa mahitaji ya kimsingi katika nyimbo zake. Hebu tuone alivyolisawiri suala hili.

Katika wimbo *Taabu ni mbaya*, msanii Kariuki anasema kuwa shida ni mbaya sana. Anaeleza namna alivyoteseka kwa kuwa hakuwa na chochote. Kataika stanza ya kwanza ya wimbo huo anasema kuwa shida inapokuingilia unaweza hata ukafikiri kuwa Mungu hana maana. Anasema kuwa kwa sababu ya umaskini au shida, unaweza kujiunga hata na madhehebu ya kishetani bila kushurutishwa na yeyote. Hebu tazama mishororo fuatayo kutoka stanza hiyo.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

*Taabu kweli ni mbaya, ikikwingilia unaweza hata kufikiria Mungu hana maana*

*Taabu kweli ni mbaya, ikikuchagua unaweza kuingia bunge la shetani bila rigging*

Katika stanza ya tatu ya wimbo huo, mwimbaji anaeleza jinsi alivyokuwa akitembea kutoka Mathare hadi Industrial Area, Nairobi, kwa kukosa pesa za nauli. Alikuwa hana kazi hivyo alikuwa anaenda kutafuta kazi. Anasema kuwa alikuwa na viatu jozi moja tu ambavyo vilikuwa vimeraruka mpaka akalazimika kuomba viatu vilivyotengenezwa kwa tairi kuukuu kutoka kwa Wamaasai. Tazama stanza hiyo hapa.

*Hebu fikiria kutoka Mathare mpaka Industrial Area kutafuta kazi*

*Hebu fikiria kutoka Mathare mpaka Industrial Area kutafuta kazi*

*Kiatu ni pair moja na kimepanua mdomo ni kama samaki*

*Shetani ashindwe*

*Mpaka nikaamua na nikaomba akala kwa Maasai Athi River*

*Mpaka nikaamua na nikaomba akala kwa Maasai Athi River*

Katika stanza ya nne, anasema kuwa alikuwa na surauli moja na shati moja ambazo ndizo alikuwa akivaa wikendi. Ilimbidi alifue shati hilo usiku lau sivyo asingepata shati la kuvaa siku iliyofuata na hivyo angelazimika kukaa pale nyumbani. Hebu tazama stanza hiyo hapa.

*Suruali ni pair moja, shati ni pair moja na ndiyo my Sunday best Hebu fikiria*

*Suruali ni pair moja, shati ni pair moja na ndiyo Jumapili best*

*Hebu fikiria*

*Kuosha ni usiku nisiposafisha kesho yake sitatokea, nivae nini?*

*Kuosha ni usiku nisiposafisha kesho yake sitatokea, zero-grazing*

Katika wimbo *Muthoni kifagio*, mwimbaji anasema kuwa walipokutana na Muthoni, Muthoni alikuwa amekonda na kudhoofika sana kiasi kwamba hakuna mwanamume mwingine angemfikiria. Hali hii ya kiafya ya Muthoni ilitokana na taabu alizozipitia Muthoni kwani alipoishi kwa KK alipokula vizuri aliweza kunawiri vizuri. Hebu tazama stanza ya 3 ya wimbo huo.

*I can remember the day tulionana na wewe*

*Ulikuwa very thin and worn out if I remember*

*Sidhani kama kuna mwanaume angekufikiria*

*Na mimi nikakulisha mpaka ukamea madiaba*

*Sasa huambiliki wala husemezeki*

*Kazi niliyofanya upate shape umesahau*

Katika stanza ya mwisho ya wimbo *Kuuma wauma gwakwa (Tangu ulipotoka kwangu)*, mwimbaji anasema kuwa mke aliyemwacha alifikiri kuwa mwimbaji angeangamia iwapo angemwacha. Hata hivyo mwimbaji anamwambia kuwa yeye sasa ni tajiri. Inaonyesha kuwa mwimbaji alikuwa maskini hapo awali na hivyo mke akamtoroka kwa sababu hiyo. Hebu tazama stanza hiyo hapa.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1419

| Asilia | Tafsiri |
|---|---|
| *Coka urirage nduru wandikwe ni mwiruguo* | Rudi uajiriwe na mke mwenza kuwinda kuchakulo |
| *Riu ninaumire wandiga* | Nilitajirika uliponiacha |
| *Wonaga ta wamberia* | Ulifikiri ningeangamia ukienda |

**Uhalifu**

Uhalifu unahusishwa na ukosefu wa usalama pale ambapo baadhi ya watu wanajihusisha na mambo ambayo yanahatarisha maisha ya wengine na pia mali yao. Mwimbaji Kariuki amelishughulikia suala hili katika nyimbo zake.

Katika wimbo Ngoma bila nguo, msanii anatupa muktadha ambapo watu wanaojiburudisha wanavamiwa na majambazi na kuibiwa nguo zao na vitu vingine. Tukio kama hili ni mfano mwafaka wa uhalifu au ukosefu wa usalama. Vinginevyo watu wanapaswa kujiburudisha bila tatizo lolote. Tazama mishororo hii kutoka wimbo huo.

*Ilikuwa saa nane ya usiku*

*Nikasikia kila mtu lala chini*

*Tukaamrishwa kila mtu atoe nguo*

*Nguo zetu zote wakakusanya*

*Pesa zetu zote wakabeba*

*Manguo zetu wakatutupia kwa sakafu*

**Mawaidha**

Msanii Newton Kariuki amelishughulikia suala la mawaidha katika nyimbo zake. Kupitia nyimbo hizi anajaribu kuwaelekeza wanajamii kuhusu baadhi ya mambo yakuzingatia ili waishi vyema au yale ambayo wanastahili kuepuka. Hebu tuone alivyoliwasilisha suala hili.

Katika stanza ya tatu ya wimbo *Murivua ni muka (Anayepigwa na mkewe)*, msanii Kariuki anaasa kuwa sio vyema kuchimba shimo nje ya nyumba. Ni wazi kuwa msanii huyu halirejelei shimo la kawaida bali mambo ambayo yanaweza kuleta matatizo. Anawazindua wanajamii kuwa kuna mambo ambayo iwapo watayafanya bila shaka watapata matatizo makubwa. Hebu tazama stanza hiyo.

| Asilia | Tafsiri |
|---|---|
| *Irima iriku ritwinjagwa thome* | Shimo kubwa halichimbwi nje |
| *Irima iriku ritwinjagwa thome* | Shimo kubwa halichimbwi nje |
| *Na wi kirimu we wenjire ria viti ikumi* | We u mjinga ulichimba la futi kumi |
| *Taroria riu we wagurire mundu murume Na aka mekuo engi ukuthanagirwa watakiondo* | Angalia sasa ulioa mwanamume Na wanawake ni wengi unakunjwa kama chondo |

Katika stanza ya nne, anasema kuwa ni muhimu watu kuvumilia mambo yanayowahusu. Anatumia mfano wa mnyama anayezaa moto kuwa atalazimika kuuramba moto huo kama wanyama wafanyavyo kwa watoto wao. Kwa maoni yake, iwapo wewe ndiye uliyejisababishia hali fulani ni sharti uishughulikie mwenyewe. Pia anaonya kuwa mchimba kisima huingia mwenyewe. Hebu tazama mishororo ifuatayo ya stanza hiyo.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

| Asilia | Tafsiri |
|---|---|
| *Yaciara mwaki nwanginya igacuna* | Mnyama akizaa moto ni lazima alambe |
| *Na mwinja kithima niwe ukirikaga* | Mchimba kisima huingia mwenyewe |
| *Niwe ukirikaga* | Huingia mwenyewe |

Katika wimbo *Urathi wina kieva (Utabiri wenye huzuni),* msanii Kariuki ametumia kauli za mawaidha kwa wanajamii wake katika takribani kila stanza. Kichwa cha wimbo huu, yaani *Utabiri wenye huzuni*, ni mfano wa kuwaelekeza wanajamii ili waweze kubadili mienendo yao iwapo wanataka kufanikiwa maishani. Kwa mfano, anatabiri kuwa iwapo wanajamii hawatajukumika, hawatakuwa na viongozi kutoka jamii yao. Pia, anasema kuwa wanajamii wasipochunga, lugha ya Kimbeere itakufa. Stanza hizi zimeonyeshwa katika sehemu inayoshughulikia maudhui ya uongozi na siasa.

Katika wimbo *Muthoni kifagio*, Newton Kariuki anaelekeza kuwa uhusiano wowote unahitaji uaminifu. Kukosekana kwa uaminifu katika upande wa Muthoni kulisababisha uhusiano kati ya KK na Muthoni kusambaratika. Anawahimiza wale walio na uhuisiano wa kimapenzi wawe na uaminifu ili wasiambukizwe ugonjwa wa UKIMWI. Hebu tazama stanza mbili za mwisho za wimbo huo.

*Urafiki siku hizi unahitaji uaminifu*

*Na bado naona wewe ni kifagio ya City Council*

*Muthoni niondokee sitaki ukifa nikufuate*

*Hujali kufungwa na karatasi ya nylon Kenyatta*

*Chunga maisha mami, adhabu iko duniani*

*Usipogongwa na gari utagongwa na UKIMWI*

*Tukipendana Wayua, jaribu uaminifu*

*Tukipendana Muthoni, jaribu uaminifu*

*Tukipendana Kamene, jaribu uaminifu*

*Usipogongwa na gari utagongwa na UKIMWI*
*Usipogongwa na gari utagongwa na UKIMWI*

*Aiiiiii mama, utagongwa na UKIMWI*

*Aiiiiii mama, utagongwa na UKIMWI*

Katika wimbo *Mke ni bahati*, msanii Kariuki anawaasa wanaume waliooa wawavumile wake wao hata kama wana tabia zisizopendeza kwani waliapa kuwa wataishi nao milele. Anaelekeza kuwa wanaume wana jukumu la kutekeleza kuhakikisha wake wao wanabadili tabia zao mbaya ili kuwawezesha kuishi inavyotakikana. Hebu tazama stanza zifuatazo za wimbo huo.

*Kumbuka uliapa utaishi na yeye milele*

*Sasa amekwisha breki*

*Brother vumilia upelekwe mbio kama magari ya miraa*

*Ndugu usifikiri sisi tulibahatika*

*Tukaoa wazuri*

*Wale tunao nyumbani*

*Wengi ni recondition kama magari ya Dubai ii*

*Kwa hivyo ukioa usifikiri umefaulu*

*Lazima ubomoe engine*

*Yaani tabia zake*

*Uweke ring mpya*

*Ndio mpate kuishi iii*

Katika wimbo *Taabu ni mbaya*, Newton Kariuki anawaasa watu kuishi kwa heshima na kila mtu hata wale ambao hawana chochote. Hii ni kwa sababu hali zao hazitadumu hivyo milele. Anauliza iwapo tuliwadharau watu fulani kwa sababu ya hali yao

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1419

duni na mambo yabadilike na kisha tuwe tunahitaji usaidizi wao baadaye tutafanya nini. Hebu tazama stanza ifuatayo.

*Brother ukifanikiwa tenda wema kwa wale unawaacha nyuma usiwadharau*

*Wahenga walisema aliye juu siku moja mngoje chini atashuka*

*Kumbuka siku moja utateremka na wale unadharau watapanda*

*Na kama uliwadhulumu mkikutane ukiteremka wakipanda hautaamini Na kama uliwadhulumu mkikutane ukiteremka wakipanda hautaamini*

Katika stanza ya mwisho ya wimbo huo, msanii anawahimiza watu kuwa wajitegemee na wasifikiri kuwa watafaidi mafanikio ya wenzao. Tazama mishororo ifuatayo ya stanza hiyo.

*Bahati ya mwenzio usiilalie, kumbuka akili ni nywele na uko na zako*

*Bahati ya mwenzio usiilalie, kumbuka akili ni nywele na uko na zako*

**Ukimwi**

Katika wimbo Muthoni kifagio msanii Kariuki anawaonya wale walio na uhusiano wa kimapenzi wawe waaminifu kwa wenzao ili wasije wakapatwa na ugonjwa wa UKIMWI. Hebu tazama stanza zifuatazo.

*Urafiki siku hizi unahitaji uaminifu*

*Na bado naona wewe ni kifagio ya City Council*

*Muthoni niondokee sitaki ukifa nikufuate*

*Hujali kufungwa na karatasi ya nylon Kenyatta*

*Chunga maisha mami, adhabu iko duniani*

*Usipogongwa na gari utagongwa na UKIMWI*

*Tukipendana Wayua, jaribu uaminifu*

*Tukipendana Muthoni, jaribu uaminifu*

*Tukipendana Kamene, jaribu uaminifu*

*Usipogongwa na gari utagongwa na UKIMWI Usipogongwa na gari utagongwa na UKIMWI*

*Aiiiiii mama, utagongwa na UKIMWI*

*Aiiiiii mama, utagongwa na UKIMWI*

**Dini na Imani**

Msanii Newton Kariuki amelisawiri suala la dini na imani katika nyimbo zake. Kwa namna fulani, ameitumia dini kama kigezo cha maadili katika jamii. Hebu tuone alivyolisawiri suala hili.

Katika wimbo *Urathi wina kieva (Utabiri wenye huzuni)* msanii huyu anatumia hadithi ya wana wa Israeli na jinsi Musa alivyowaongoza kutoka Misri. Hata ingawa hadithi hii inaweza kuwa na maana fiche, ukweli kwamba ameitumia ni ithibati ya msimamo wa kiimani na dini. Hebu tazama mishororo ifuatayo ya stanza ya kwanza ya wimbo huo.

| Asilia | Tafsiri |
|---|---|
| *Musa atumwa ni Ngai agire ciana ukombori* | Musa alitumwa na Mungu aendee watoto utumwani |
| *Musa atumwa ni Ngai agire ciana Misiri* | Musa alitumwa na Mungu aendee watoto Misiri |
| *Agicokeria Ngai nii timbota* | Akamwambia Mungu kuwa hangeweza Hapa panastahili mtu jasiri |
| *Vandu ava varenda mundu uri na kanua karuu* | |
| *Akirwa tanguve Haron agutware* | Akaambiwa apewe Haruni waende pamoja |

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Katika wimbo *Mke ni bahati*, msanii Kariuki anataja ndoa ambazo hufanywa makanisani kupitia harusi. Mandhari ya kanisani na suala la harusi ni dhana zinazoambatana na dini ya Kikristo. Katika wimbo huu pia anamtaja mkewe Loti ambaye anajulikana katika Biblia kwa kutozigatia maagizo na hivyo kugeuka na kuwa jiwe la chumvi. Hebu tazama stanza ifuatayo ya wimbo huu.

> *Wengi mnaooa kwa harusi makanisani*
>
> *Wameshinda wazazi wao*
>
> *Wengi hawajaokoka*
>
> *Wengi ni vichwa ngumu hata kuliko bibi ya Loti iii*

Katika wimbo *Taabu ni mbaya*, mwimbaji anamshukuru Mungu kwa kumtoa kwenye shida kubwa. Anasema kuwa shida inaweza kumfanya mtu akafikiri kuwa Mungu hana maana. Hii inaonyesha kuwa kulingana na mwimbaji Mungu ana maana. Hebu tazama mishororo ifuatayo ya stanza ya kwanza na ya pili ya wimbo huo.

> *Taabu kweli ni mbaya, ikikwingilia unaweza hata kufikiria Mungu hana maana Taabu kweli ni mbaya, ikikuchagua unaweza kuingia bunge la shetani bila rigging KK nikikumbuka pahali nilipokuwa na pahali nilipo sasa Mungu asifiwe KK nikikumbuka pahali nilipokuwa na pahali nilipo sasa Mungu asifiwe*

Katika stanza ya mwisho ya wimbo huu, mwimbaji anasema kuwa aliponunua gari lake watu wengine walisema kuwa alikuwa amejiunga na wanaomwabudu shetani. Anamshukuru Mungu kwa kuwa shida haina mizizi. Kauli hii inaonyesha imani ya watu mbalimbali. Hebu tazama mishororo ifuatayo ya stanza hiyo.

> *Brother taabu ni mbaya lakini mimi nashukuru Mungu kwa kuwa haina mizizi*
>
> *Kama ni mimi leo ninaendesha gari langu kujinunulia mimi mwenyewe*
>
> *Hata ingawa wengine niliponunua walisema mimi ni member wa devil worshippers*

## HITIMISHO

Makala hii imedhihirisha kuwa maudhui katika nyimbo teule za Newton Karishi yanaweza kuwekwa katika vikoa vitatu. Hivi ni pamoja na: kisiasa, kijamii na kiuchumi. Maudhui yaliyoangazia masuala ya kijamii ni mapenzi, ndoa na familia, migogoro katika ndoa, kuporomoka kwa maadili, uhalifu, mawaidha, na ukwimwi. Isitoshe, maudhui yaliyohusu masuala ya kiuchumi ni umaskini. Waaidha, aliangazia mambo ya dini na imani. Hatimaye, masuala ya kisiasa kama vile uongozi na siasa. Ifahamike kuwa kutokana na matokeo haya ni bayana kuwa sampuli teule ilitawaliwa na maudhui ya kijamii. Huanda kutokana na mahitaji ya hadhira lengwa.

## MAREJELEO

Crystal, D. & Davy, D. (1969). *Investigating English Styles.* London. Longman.

Davy, D. (1969). *Investigating English Style*; Indiana University Press, Bloomington, Indiana.

Derrida, J. (1973). *Speech and Phenomena, and other Essays on Husserls Theory of Signs*, Evanson: North-Western University Press.

Mbogo, N. (2008). Mabadiliko ya Maudhui Kiwakati katika Nyimbo za Harusi za Jamii ya Waembu (Unpublished Thesis), Kenyatta.

Mugenda, O. M., & Mugenda, G. A. (1999. *Research Methods: Quantitativeand Qualitative Approaches.* Nairobi; Acts Press.

Mutwiri, G. (2005). Mitazamo ya Utendakazi wa nyiso katika Jamii ya Watigania. Tasnifu ya Uzamili: Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1419

Mweteri, I. (*2021). Urejeleano katika Utunzi wa Kamusi za Kiswahili: Uchanganuzi Linganishi wa Kamusi za Lugha Moja.* Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).

Njogu, K. & Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa fasihi, nadharia na mbinu.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Saussure, F., (1966). *Course in general linguistics*. In Bally, C. & Sechehaye, A. New York: McGraw-Hill.

Saussure, F. (1983). *Course in General Linguistics (Trans Roy Harris)* London. Duckworth.

Simiyu, F. (2007). Maendeleo na Mabadiliko katika Nyiso za Wabukusu: Lugha wa Maudhui (Unpublished Thesis), Kenyatta University.

TUKI (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu 4th Edition*, Oxford.

Wafula, R. & Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitilia, K. (2004). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi.* Nairobi: Focus Publications Ltd.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.